

# SOLSTICE


## Roboti za baharini zinatusaidia katika



Kujifunza kuhusu hali ya hewa
na mwenendo wa bahari




Kuyaelewa mazingira ya bahari




Kufikia na kujifunza kuhusu mazingira
ya bahari kuu

# Ukiiona roboti mahali





USIICHUKUE




USIJARIBU KUIGUSA WALA KUIKAMATA

Ukiikuta roboti imekwama mahali katika kina kifupi wasiliana nasi kupitia +255 713408628 / +255 767384438 ukitueleza mahali ilipo



# Roboti za baharini katika ukanda wa pwani ya Tanzania




Roboti za baharini zinasafiri ndani ya maji kuanzia tabaka la maji ya juu hadi kufikia zaidi ya mamia ya mita kwenda chini, na zinaweza kutembelea maeneo mbali mbali ya baharini bila kuongozwa.

Katika safari zake, roboti hizi za baharini hufanya vipimo mbalimbali na hivyo kuwasaidia wanasayansi kuelewa jinsi bahari inavyobadilika.

Kila roboti ina kazi yake maalumu. Kuna zinazopima joto na virutubisho, zingine zinapima jinsi matabaka ya maji baharini yanavyochanganyika, wakati nyingine zina uwezo wa kutambua uwepo wa samaki.

Roboti zinazotumika Tanzania zitawasaidia wanasayansi wa hapa nchini kuelewa juu ya utunzaji wa hazina ya samaki, na jinsi inavyoathiriwa na mwenendo wa mabadiliko ya pepo za kusi na kaskazi, pamoja na mabadiliko ya muda mrefu ya tabia nchi.

Roboti za baharini ni vyombovinavyojiendesha vyenyewe vinavyotusaidia kuielewa bahari.

# Tunafanya kazi kwa mashirikiano

solstice-wio.org